

UVUVI

Mnyeti ahimiza uwekezaji viwanda vya samaki

Victor Tullo, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti amewataka wananchi kufanya uwekezaji wa viwanda vya kuchakata samaki ili kuongeza mnyororo wa thamani katika sekta hiyo.

Alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akifunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri) kutumia data zito-kanazo na tafiti za uvuvi ili kuleta tija katika uchumi.

"Kwa sasa tunahamasisha watu kuanza kufungua viwanda. Hatuwezi kusafirisha samaki kwenda nje ya nchi, lazima tusafirisha minofu ambayo imeshachakatwa kwa ajili ya matumizi ya mlaji," alisema.


Alibainisha kwamba sekta hiyo bado ina mchango mdogo katika pato la Taifa, ikichangia takriban asilimia zisizozidi saba.

Mtafiti na Kaimu Mkurugenzi wa Utafiti na Uratibu, Dk Mary Kishe alisema mafunzo hayo yalijikita kwenye mambo makuu makubwa, ikiwemo namna takwimu za kitafiti zitakavyosaidia uendelevu wa rasilimali za uvuvi.

"Pia tumeangazia ni namna gani tutawashirikisha watunga sera na wale wanaosimamia rasilimali za uvuvi," alisema Dk Kishe.

Aliongeza kuwa wameangalia namna takwimu zitakavyotoa uhalisia wa mchango wa sekta ya uvuvi katika uchumi wa Taifa.

"Tumegundua baadhi ya upun-



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti akizungumza wakati wa kufunga mafunzo ya kuwajengea uwezo wataalamu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (Tafiri). Jijini Dar es Salaam jana. Picha na Victor Tullo


gufu, tumebainisha na tumeona umuhimu wa kuuziba," alisema.

Aidha, alisema wamefanikiwa kuwaonyesha washirika walio-andaa mafunzo hayo, Shirika la Chakula na Kilimo (FAO) na Chuo Kikuu cha Duke cha nchini Uingereza takwimu zilizopo na umuhimu wake.

Naye, Ofisa Uvuvi Mkuu wa Wizara ya Mifungo na Uvuvi, Lilian Ibengwe alisema walianza kufanya kazi na FAO tangu mwaka 2017 na waliingia makubalia-

no ya kutekeleza mradi mdogo unaolenga kutengeneza mpango kazi wa kitaifa utakaoainisha changamoto za wavuvi wadogo, kuanzisha jukwaa la kina mama wavuvi na kuanzisha dawati la jinsia wizarani.

"Hayo yote tulifanikiwa kutekeleza na ndipo FAO walipoamua kufanya kazi na Tanzania na tukachaguliwa kuwa miongoni mwa nchi duniani zitakazoangazia mchango wa wavuvi wadogo," alisema Ibengwe.



"Kwa sasa tunahamasisha watu kuanza kufungua viwanda. Hatuwezi kusafirisha samaki kwenda nje ya nchi, lazima tusafirisha minofu ambayo imeshachakatwa."

Mnyeti